

Kutoa Habari Kuhusu Dhuluma kwa Mtoto katika Jimbo la Vermont

Ikiwa unashuku kwamba mtoto anadhulumwa au kutelekezwa, tafadhali piga simu kwa 1-800-649-5285 ili utoe habari - saa 24 kwa simu, siku 7 kwa wiki.

Simu ya Ulinzi wa Mtoto ya Saa 24 ya Vermont hukuwezesha kujadili wasiwasi wako kuhusu mtoto na mfanyakazi wa kijamii aliye na mafunzo kwa urahisi.

Ikiwa mtoto yuko katika hatari ya karibu, piga simu kwa 911 au kituo cha polisi kilicho karibu kwanza. Kisha, tupigie simu ili utupe habari.

Ni nani anaweza kutoa habari?

Tunawahasisha wakazi wote wa Vermont wapige simu kwa Simu ya Ulinzi wa Mtoto ili watoe habari ya wasiwasi wao kuhusu usalama wa mtoto. Watu fulani, wanaoitwa *watu wenye jukumu la kutoa habari*, wanahitajika kisheria kutujulisha kuhusu dhuluma yoyote au utelekezaji wowote wa mtoto unaoshukiwa ndani ya saa 24.

DOKEZO: Kabla ya kupiga simu, jaribu kukusanya taarifa nyingi uwezavyo (k.m., jina la mtoto, tarehe ya kuzaliwa, anwani ya nyumbani, shule au mtoa huduma ya mtoto, na majina ya wazazi).

Ulinzi wa mtoto ni shughuli ya kila mtu. Simu yako inaweza kumlinda mtoto, kuipa famili usaidizi, na hata kuokoa maisha ya mtoto!

Watu Wenye Jukumu la Kutoa Habari katika Jimbo la Vermont

Ikiwa unafanya kazi katika taaluma moja kati ya zilizoorodheshwa hapa chini, wewe ni *mtu mwenye jukumu la kutoa habari* na unahitajika kisheria kutoa habari kuhusu dhuluma au utelekezaji wa mtoto unaoshukiwa ndani ya saa 24.

- Mtaalamu wa maungo, daktari wa meno, mfanyakazi wa matibabu ya dharura, nesi mwenye leseni, mchunguzi wa kimatibabu, mtaalamu wa afya ya kiakili, daktari wa mifupa, mfamasi, daktari, daktari msaidizi, mwanasaikolojia, nesi aliyesajiliwa, daktari mpasuaji, au wahudumu wengine wa afya;
- Msimamizi wa hospitali, daktari mkufunzi, au daktari mkazi katika hospitali yoyote ndani ya jimbo;
- Msimamizi wa shule, mkurugenzi, mwalimu mkuu, mwalimu, mkutubi, mshauri wa uongozi wa shule, na watu wengine ambao huajiriwa mara kwa mara na, au

wanaoajiriwa kwa mkataba na kulipwa na, wilaya ya shule au shule huru kutoa huduma kwa wanafunzi;

- Mfanyakazi wa huduma za watoto, afisa wa polisi, ofisa wa majaribio, mfanyakazi wa kijamii, au makasisi wa kanisa;
- Msimamizi na mshauri mkazi wa kambi na wa muda, au mmiliki; na
- Mfanyakazi, kontrakta, au mdhamini wa Uajenti wa Huduma kwa Binadamu anayeweza kuwasiliana na wateja.

Bofya hapa ikiwa una jukumu la kutoa habari.